

Shamba la Mzabibu, Mzabibu, na Mzeituni

Kama ungesawa kusafiri kuenda milima ya kati ya nchi ya Israeli leo katika msimu unaofaa, utapata wingi wa mizabibu wenye matunda. Matunda ya mizabibu, kwa kweli, ni zabibu, ambayo juisi yake ikichachwa hutoa divai. Mzabibu na shamba la mizabibu ni kawaida ya rutuba ya kilimo ya Israeli na hutumika kama picha nzuri kwa ardhi lake.

**Na nimwimbie mpenzi wangu, wimbo wa mpenzi wangu
Katika habari za shamba lake la mizabibu.
Mpenzi wangu alikuwa na shamba la mizabibu
kilimani penye kuzaa sana;
Akafanya handaki kulizunguka pande zote,
Akatoa mawe yake,
Akapanda ndani yake mizabibu ulio mzuri,
Akajenga mnara katikati yake,
Akachimba shinikizo ndani yake;
Akatumaini ya kuwa utazaa zabibu,
Nao ukazaa zabibu-mwitu.**
(Isaya 5:1-2)

Shamba La Mzabibu Lisilofaa

Somo hili la shamba la mizabibu linafunua kwamba Mungu alitarajia taifa lake teule kuzaa matunda – katika maneno mengine, kutekeleza kazi Yake na kusimamia haki. Kwa bahati mbaya ulizaa matunda, lakini matunda yalikuwa machungu na ya mwitu (Tazama Isaya 5:2: “Nao ukazaa zabibu-mwitu.”)

“Na sasa, enyi wenyeji wa Yerusalem, nanyi watu wa Yuda, amueni, nawasihi, kati ya mimi na shamba langu la mizabibu. Je! Ni kazi gani iliyoweza kutendeka ndani ya shamba langu la mizabibu nisiyoitenda? Basi, nilipotumaini ya kuwa litazaa zabibu, mbona lilizaa zabibu-mwitu? Haya basi, sasa nitawaambieni nitakalolitenda shamba langu la mizabibu; nitaondoa kitalu chake, nalo litaliwa; nitabomoa ukuta wake, nalo litakanyagwa; nami nitaliharibu; wala halitapogolewa wala kulimwa; bali litamea mbigili na miiba; nami nitayaamuru mawingu yasinyeshe mvua juu yake. Kwa maana shamba la mizabibu la BWANA wa majeshi ndio nyumba ya Israeli, na watu wa Yuda ni miche wake wa kupendeza; akatumaini kuona hukumu ya haki na kumbe! Aliona dhuluma” (Isaya 5:3-7).

Kifungu hiki kinatumia mchezo juu ya maneno: Maneno ya Kiebrania kwa *hukumu* na *ukandamizaji* yanaonekana kuwa sawa, kama vile yale ya *haki* na *kulia*. Yesu alisema, “Ndiposa kwa matunda yao mtawatambua” (Mathayo 7:20). Somo hili la shamba la mizabibu linaweza kuchukuliwa kibinagsi, likituhimiza kuchunguza “matunda” yetu.

Mistari hii ya Isaya inarejelea Israeli, “shamba la mizabibu” lililo tasa. Kwa upande mwingine, Yerusalemu na Hekalu hurejelewa katika Biblia kama “mzabibu.”

Katika karne ya nane KK Bwana aliomboleza kuitia Isaya juu ya hali tasa ya shamba la mizabibu (Israeli) na mzabibu (Yerusalemu).

Wakati Mungu aliwaongoza watu wake kuingia Nchi ya Ahadi (shamba la mizabibu) chini ya uongozi wa Yoshua, Aliwaondoa mataifa wasiomcha Mungu ambao miyo yao yalikuwa kama jiwe Kwake. Basi Alipanda Nchi ya Ahadi na “mzabibu mzuri zaidi.” Mnara alioujenga katikati yake inawakilisha Hekalu la kwanza lililojengwa na Mfalme Sulemani.

Mungu alifanya mambo ya kushangaza kwa Israeli. Aliwaongoza watu wake kutoka Misri kuitia jangwani na kuingia Nchi ya Ahadi. Aliondoa mawe (wapagani) na akapanda Israeli kama mzabibu mzuri. Israeli ni shamba la mizabibu la Mungu, sio tu kwa sababu Mungu anaipenda, bali pia kwa sababu aliandaa ardhi hiyo kwa bidii na kuipanda. Pia aliilinda kwa uangalifu. Kwa njia hii, mithali unaelezea uchaguzi wa Mungu wa Israeli kama taifa (Kumbukumbu la Torati 7:7-11) na utunzaji wake kwake. Kama ilivyo kwa shamba lolote la mizabibu, Mkulima wa mizabibu hufanya kazi yake yote kwa matarajio ya mavuno yenye matunda mengi.

Katika Zaburi ya 80, tunaona mfano mwingine wa mada sawa. Mtunga Zaburi anaelezea Kutoka kwa lugha ya shamba la mizabibu: “Uiletta mzabibu kutoka Misri: Ukawafukuza mataifa ukaupanda. Ulitengeneza nafasi mbele yake, nao ukatia mzizi sana ukaijaza nchi” (Zaburi 80:8-9).

Tunadhani Mungu anatarajia nini kutoka kwetu, baada ya kila kitu ambacho ametufanyia? Je! Mungu anaweza kuwa anasubiri kuona matunda yetu? Mara tatu Mtunga Zaburi anamwomba Mungu “kuturudisha” (Zaburi 80:3,7,19). Toba inajumuisha kujinyenyekesa na kumrudia Mungu ili kupokea msamaha wake na urejesho. Tunaposimama mbele ya Yesu Kristo, atakuwa anatafuta tunda – “tunda la Roho.” “Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi: juu ya mambo kama hayo hakuna sheria” (Wagalatia 5:22).

Kazi ya Roho Mtakatifu ndani yetu huzaa tabia hizi, ambazo hupatikana katika asili ya Kristo. Sisi wenyewe hatuwezi kuzipata. Ni mazao zinazohamasishwa na Roho wa Kristo. Ikiwa tunataka tunda liwe ndani yetu lazima tuunganishe maisha yetu kwa Yake. “Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu. Kama vile tawi lisivyoweza kuzaa matunda peke yake, lisipokaa ndani ya mzabibu; kadhalika nanyi, msipokaa ndani yangu. Mimi ni mzabibu, nanyi ni matawi, akaaye

ndani yangu, nami ndani yake, huyo huzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamwezi kufanya neno lolote” (Yohana 15:4-5).

Na kwa hivyo unabii huu wa Isaya 5:3-6 ultimia. Mungu aliuondoa mkono wake wa ulinzi, baraka, na rehema kutoka kwa Israeli, ili mataifa yenye uhasama (Waashuri na Wababeli) wamwangukie kama wanyama wa porini. Kwa sababu walikataa kujisalimisha wenyewe kwa Bwana Mungu na kumfuata kwa moyo wote, walivutwa katika ulimwengu, mawazo yao yakiwa juu ya mambo na njia za kidunia.

Yerusalemu: Mzabibu Uliokataliwa

Katika karne ya sita KK, nabii Ezekieli alionekana kwenye eneo kwa mara ya kwanza. Kufikia wakati huu shambulio la kwanza la Babeli lilikuwa limetokea na baadhi ya Waisraeli walikuwa wameondolewa kwenye ardhi.

Nabii Ezekieli aliishi miaka 150-200 baadaye kuliko Isaya. Ingawa Isaya aliishi Israeli, Ezekieli alikuwa mateka wa Babeli, unabii wa Ezekieli ulifuata unabii wa Isaya bila usumbufu au upinzani.

Walakini, Ezekieli hakutabiri tu juu ya “shamba la mizabibu” (Israeli), bali pia juu ya “mzabibu” (Yerusalemu). Ezekieli anaandika, ‘Neno la BWANA likanijia, kusema, Mwanadamu, mzabibu una sifa gani kuliko mti mwagine, au tawi la mzabibu lililokuwa kati ya miti ya msituni? Je! Mti wake waweza kutwaliwa, ili kufanya kazi yoyote? Watu waweza kufanya chango kwa huo, ili kutundika chombo chochote? Tazama, watupwa motoni kwa kuni moto umeziteketeza ncha zake zote mbili, nao umeteketea katikati, je! Wafaa kwa kazi yoyote? Tazama, ulipokuwa mzima, hauku faa kwa kazi yoyote; sembuse ukiisha kuliwa na moto, na kuteketea; je! Waweza kufaa kwa kazi yoyote? Basi Bwana MUNGU asema hivi; kama mizabibu kati ya miti ya msituni, niliyoupa moto uwe kuni, ndivyo nitakavyowatoa wakao Yerusalemu. Nami nitaukaza uso wangu juu yao; nao watatoka motoni, lakini moto utawateketeza; nanyi mtajua ya kuwa mimi ndimi Bwana, nitakapoukaza uso wangu juu yao. Nami nitafanya nchi kuwa ukiwa, kwa sababu wamekosa, asema Bwana Mungu” (Ezekiel 15:1-8).

Katika sura ya 15 hadi 17, Ezekieli anatoa ushahidi zaidi kwamba Mungu alikuwa anaenda kuharibu Yerusalemu. Katika hadithi ya mzabibu, tunaona ilikuwa haina maana mwanzoni na hata ya thamani kidogo baada ya kuchomwa moto. Wakazi wa Yerusalemu walikuwa wasio na maana kwa Mungu kwa sababu ya ibada yao ya sanamu, kwa hivyo wataangamizwa na miji yao kuteketezwa. Tusithubutu kujiruhusu kukaa kimya na kutozaa matunda kwa Mungu. Tunahitaji kuwa shughuli ya Baba yetu.

Mfano hapa hauwezi kuwa wazi. Mungu hakuwa na matumizi zaidi kwa Yerusalemu. Kama mzabibu, ilishindwa kuzaa matunda, na hata kuni za mzabibu zilikuwa bure, isipokuwa

kuchomwa moto (Ezekiel 15:5). Kuchomwa ilikuwa hatima ambayo ilianguka juu ya hiyo kizazi, ilivyoruhusiwa na mkulima wa Mzabibu.

Baraka kuu — ya kutumiwa na Mungu kama shahidi kwa mataifa — ilipotezwa kwa Yerusalem, kwa hivyo hakukuwa na haja tena ya jiji au Hekalu. “Walete vipofu walio na macho, na viziwi walio na masikio. Na wakusanyike mataifa yote, khabila zote wakutanike; ni nani mionganoni mwao awezaye kuhubiri neno hili na kutuonyesha mambo ya zamani? Na walete mashahidi wao, wapate kuhesabiwa kuwa na haki; au na wasikie, wakaseme, Ni kweli. Ninyi ni mashahidi wangu, asema BWANA, na mtumishi niliyemchagua; mpate kujua, na kuniamini na kufahamu ya kuwa mimi ndiye; kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwapo mwingine. Mimi, naam, mimi, ni BWANA, zaidi yangu mimi hapana mwokozi” (Isaya 43:8-11).

Lakini Israeli ilifanya kinyume kabisa. Aliinama mbele ya sanamu za mataifa na kuwaabudu badala ya kushuhudia kwa neno na tendo kwamba walikuwa watoto na mashahidi wa Mungu wa kweli.

Chini ya Yeroboamu II, Israeli ilifanikiwa na kupata nguvu za kijeshi na kiuchumi. Lakini kadiri taifa lilivyofanikiwa, ndivyo watu walivyopenda sanamu zaidi. “Ingawa Israeli alikuwa tajiri — mzabibu utoao matunda yake! Lakini kwa kadiri ya wingi wa matunda yake, kadiri iyo hiyo ameongeza madhabahu za miungu yao ya kigeni. Mavuno yalipokuwa mengi ndivyo walivyojenga sanamu” (Hosea 10:1).

Kujihusisha na dhambi daima ni hatua mbaya na mwishowe huleta utasa. Mwanzoni, Israeli ilizaa matunda, lakini baadaye ikajihuhsisha na Ashuru na Babeli. Matokeo yalizaa “zabibu” zilizopooza kwenye shamba la mizabibu ambazo zilianguka kutoka kwenye mzabibu, na hazikuweza tena kuvunwa ili kutengeneza divai nzuri. Israeli hakuwa mwaminifu kwa Mungu wake; kwa hivyo, Hekalu lilipoteza haki yake ya kuishi. Israeli, Yerusalem, na Hekalu, mara tu Mungu alipowapa mataifa, wote walianguka kwa moto.

Wababeli walichoma “shamba la mizabibu” na kisha “mzabibu” (Yerusalem na Hekalu) kwa njia ile ile kama ilivytobiriwa na manabii.

Matunda mabaya sio jukumu la mtunza mizabibu, ambaye alijali sana kupanda na kutunza mzabibu (Ezekiel 17:5-6). Mzabibu yenyewe ndio una makosa. Ilizalisha zabibu mbaya licha ya faida zote ilizokuwa nazo.

Kwa sababu matunda ambayo shamba la mizabibu lilizalisha halikuwa nzuri, Mungu atakuja katika *hukumu* na kuharibu shamba la mizabibu. Katika moja ya matumizi ya kibiblia ya kupendeza zaidi ya picha ya shamba la mizabibu, Kumbukumbu la Torati inasisitiza sio tu hukumu lakini pia uhusiano kati ya dhambi za watu wa Mungu na zile za jiji maarufu la Sodoma: “Maana, mzabibu wao ni mzabibu wa Sodoma, nao ni wa mashamba ya Gomora. Zabibu zao ni

zabibu za uchungu, vichala vyao ni vichungu. Mvinyo yao ni sumu ya majoka, uchungu mkali wa nyoka” (Kumbukumbu la Torati 32:32).

Wababeli walikuja kwa mara ya kwanza na kuishika Israeli mnamo 605 KK. Wakati huo nabii Danieli alichukuliwa kwenda Babeli.

Jeshi la Mfalme Nebukadreza lilikuja kwa mara ya pili mnamo 597 KK. Wakati huo Ezekieli alipelekwa katika nchi ya Wakaldayo. Kwa hivyo neno lilitimizwa: “Moto umeziteketeza ncha zake mbili.” Lakini Yerusalemu wakati huo ilikuwa imeokolewa. Moto ulikaribia sana jiji, hata hivyo, “na kupiga katikati.” “Tazama, watupwa motoni kuwa kuni; moto umeziteketeza ncha zake zote mbili” (Ezekiel 15:4). Hatimaye wakati wa uharibifu wao wa mwisho kwa moto ulikuja mnamo 586 KK. Kwa maana halisi ya neno ardhi ilifanywa ukiwa. “Kwa sababu wamekosa, asema BWANA MUNGU” (aya 8).

Marejesho Yanaleta Rutuba Kwa Mzabibu

Wakati mwingine inaweza kuonekana kuwa ngumu kuelewa, lakini rehema ya Mungu ni kwa kila mtu. Utunzaji wa Mungu kwa Wayahudi na Mataifa unakusudiwa kutuonyesha rehema Yake. Jumla ya hoja ya Paulo ni kwamba mwishowe kutakuwa na nafasi kwa Wayahudi na watu wa mataifa mengine katika mpango wa Mungu. Jinsi Mungu atakavyofanya hii ni fumbo!

Mtume Paulo katika kitabu cha Warumi anatufunulia Mungu wa Israeli, ambaye zawadi zake na wito haubadiliki. “Kwa sababu karama za Mungu hazina majuto, wala mwito wake” (Warumi 11:29). Mstari huu pia unawenza kutafsiriwa “marupurupu na mwaliko wa Mungu [aliyopewa Israeli] haiwezi kuondolewa kamwe. Hii inamaanisha kwamba watu wake ni wapendwa kwa ajili ya Baba, ingawa walishindwa na hawakuwa waaminifu na hata wakajidhihirisha wenyewe kuwa maadui wa Injili. Kwa sababu ya hii Bwana alifanya ahadi ifuatayo. “Na wao wakaao chini ya uvuli wake watarejea; watafufuka kama ngano, na kuchanua maua kama mzabibu; harufu yake itakuwa kama harufu ya divai ya Lebanoni. Efraimu atasema, Mimi nina nini tena na sanamu? Mimi nimeitika, nami nitamwangalia. Mimi ni kama mberoshi wenye majani mabichi. Kwangu mimi yamepatikana matunda yako” (Hosea 14:4, 7-8).

Hebu fikiria, “shamba la mizabibu” na “mzabibu” yote yakichomwa. Israeli, Yerusalemu, na Hekalu liliaribiwa. Hata “ukuta” na “uzio” zilibomolewa.

Mbona mzabibu uliochomwa haukuteketea? Kumbuka kile Hosea alisema katika mstari wa 8 hapo awali: “Kwangu mimi yamepatikana matunda yako.” Ikiwa hasira na hukumu ya Mungu inawakilishwa na shamba la mizabibu liloharibiwa, haipaswi kushangaza kwamba baraka na urejesho wa Mungu zimeonyeshwa kuitia picha ya shamba la mizabibu lenye rutuba. Manabii waliogozwa na Mungu kuangalia zaidi ya hukumu kwa urejesho na kutazamwa kwa afya na

rutuba ya mizabibu. “Mara ya pili utapanda mizabibu juu ya milima ya Samaria; wapanzi watapanda, nao watayafurahia matunda yake” (Yeremia 31:5).

Katika siku zijazo, Israeli itageuka. Kugeuka kwao kutatoka kwa Masihi. “Mimi ndiye mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima” (Yohana 15:1). Kwa hivyo, taarifa tuliyosoma katika Hosea hapo awali inamtaja Masihi. Kupitia Yeye Israeli itazaa matunda na utastawi kama mzabibu unaofunika dunia nzima.

Zaburi ya 80 inakumbuka historia ya kutoka kwa Israeli kutoka Misri na maelezo ya kuchukua milki ya Kanaani. Mstari wa 11 unatuambia, ‘‘Nao uliyaeneza matawi yake hata baharini, na vichipukizi vyake hata kunako mto.’’ Hii ni dalili wazi ya eneo lililo chini ya ushawishi wa Israeli, ikipanuliwa kutoka Mto Frati hadi Bahari ya Mediterania na Daudi na Sulemani. Lakini, kisha uharibifu ukaja. “Kuta” zake zilibomolewa, “nguruwe wa msituni” waliiharibu na “hayawani wa kondeni” waliutafuna mzabibu (aya 12-13). Ashuru na Babeli wanarejelewa, na labda hata mataifa mengine machafu.

Katika aya ya 14 na 15, Mtunga Zaburi anaonekana akimsihi Mungu kurudi, kama alivyokuwa akiwahimiza watu Wake kurudi. Kusudi la kurudi Kwake ni “kuangalia na kuona” hali ya shamba la mizabibu lililoharibiwa na kuirejesha. “Ee Mungu wa majeshi, tunakusihi urudi; utazame toka juu uone, uuJulie mzabibu huu. Na mche ule ulioupanda kwa mkono wako wa kuume; Na tawi lile ulilolifanya kuwa imara kwa nafsi yako (aya 14-15). Mstari wa 15 unaweza hata kutaja baraka za Yakobo (Mwanzo 49:22), kwani Yusufu anaitwa “mti mchanga wenye kuzaa,” maana yake ni “mwana.”

Walakini, ukikata kutoka kwa mzabibu wa zamani na kuipanda ardhini, mzabibu wa zamani huishi hata ikiwa imechomwa. “Kukatwa” hii ni Mwana wa Mungu. Alizaliwa katika ulimwengu huu kama Myahudi. Alipandwa katika ulimwengu huu. Kwa hivyo “mzabibu” uliochomwa wa Israeli unaendelea kuishi ndani ya Yesu Kristo. Kumbuka kile Yesu alisema wakati wa kutokea kwake mara ya kwanza. “Mimi ni mzabibu wa kweli, na Baba yangu ndiye mkulima” (Yohana 15:1). Kwa hivyo, “mzabibu” wa kweli, aliye Yesu, anachukua nafasi ya “mzabibu” tasa, Israeli. “Kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa; na kila tawi lizaalo hulisafisha, ili lizidi kuzaa... Mtu asipokaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi, na kunyauka; watu huyakusanya, na kuyatupa motoni yakateketea” (Yohana 15:2, 6).

Yuda msaliti alijitenga na Yesu na kuangamia. Kwa wanafunzi wengine Yesu alisema, “Ninyi mmekwisha kuwa safi kwa sababu ya lile neno nililowaambia” (Yohana 15:3).

Kwa sababu viongozi wa Wayahudi hawakumtaka Yesu: “Hatumtaki huyu atutawale” (Luka 19:14). “Sisi hatuna mfalme ila Kaisari” (Yohana 19:15). Matokeo ya mienendo hii ililetä askari kutoka kwa mfalme wa Kirumi hadi Israeli. Yerusalem ulizingirwa, kutekwa, na kuchomwa moto. Na maneno ya mtunga Zaburi yanarudi kwetu kama mwangwi. “Umechomwa moto, umekatwa; kwa lawama ya uso wako wanapotea” (Zaburi 80:16).

Kupata uhakika wa wokovu

Watu wengi hupitia maisha wakijiuliza kama wataokolewa. Ingawa wamebatizwa vizuri na kupokea kuwekelewa mikono, bado wanao mashaka. Kweli, Mungu anataka nini kwa watu kabla ya kuwapa zawadi ya uzima wa milele na *uhakikisho* wa kuingia katika Ufalme? Hili ni swali zito sana, na ni muhimu kwa waumini wote kuwa na jibu la kibiblia ambalo wanaweza kuamini.

Israeli, kama mzabibu wa Mungu katika Agano la Kale, ilikuwa aibu kubwa kwa sababu ilitoa matunda yaliyooza tu; yaani, walikataa kumpa Mungu upendo na utiifu. Maandiko ambayo tumepitia tayari hutoa picha dhahiri ya kutofaulu kwa Israeli na mengi ya vifungu vya kusikitisha kwa Yesu kuzingatia.

Yesu pamoja na waumini wote “wanaokaa” ndani yake ndiye MIZABIBU YA KWELI — utimilifu wa kweli wa Mpango wa Mungu kwa watu wake. Jamii hii mpya ya watu wa Mungu — Wakristo — inatokana na Yesu Kristo na wameunganishwa naye kama matawi kwa mzabibu. Mungu Baba ndiye mtunza bustani, mkulima wa mzabibu na matawi. Hapa ndipo inakuwa ngumu, kwa sababu waumini wote wa kweli na wa uwongo wanaonyeshwa hapa kama matawi.

Matawi yanayozaa matunda ni waumini wa kweli ambao, kwa umoja wao hai katika Kristo, wanazalisha matunda mengi. Walakini, muumini wa kweli anaweza kuvunja muungano. Baba hukata kila tawi lisilozaa matunda. Wale ambao hawazalishi matunda kwa kurudi nyuma na kutomfuata Kristo wanakatwa kutoka kwenye mzabibu. Je! Mungu anatarajia tunda la aina gani kutoka kwetu? Matunda hayapungukiwi kwa kuleta wengine kwa Kristo.

Tazama mafungu haya katika Yohana sura ya 15: “Ninyi mkikaa ndani yangu, na maneno yangu yakikaa ndani yenu, ombeni mtakalo lote nanyi mtatendewa” (aya ya 7). Maombi yaliyojibowi ni matunda muhimu sana kuzalishwa katika maisha yako. Yesu anazungumza juu ya “furaha” kama matunda ambayo Anatamani kukaa ndani yetu kikamilifu. “Hayo nimewaambia, ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe” (mstari wa 11).

Anatupatia pia amri ambayo inahusisha upendo. “Amri yangu ndiyo hii, mpandane, kama nilivyowapenda ninyi” (aya ya 12). Tunapaswa kupenda kila mmoja kama vile Yesu alivyotupenda, na alitupenda ya kutosha kutoa maisha yake. Uwezekano mkubwa kwetu ni kwamba hakutakuwa na hitaji la kufa kwa sababu ya mwagine, lakini kuna njia zingine za upendo wa kujitolea, kama vile kusikiliza, kusaidia, kutia moyo, na kutoa.

“Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi: juu ya mambo kama hayo hakuna sheria” (Wagalatia 5:22-23). Utangulizi wa mtume Paulo wa neno *tunda* umejawa na maana. Maana aliyofikisha ni ya mavuno kamili ya fadhila. Tunda ni bidhaa inayotokana; inachukua muda kukua na inahitaji utunzaji na kilimo. Ni *Roho* ambaye hutoa matunda. Lazima tuchungane na Roho ili kumkaribia Mungu. Hii itaturuhusu kuonyesha

tunda la Roho. Hii kuonyeshwa kwa tunda la Roho hakutimizwi kwa matendo yetu, lakini ni kwa sababu tu Roho Mtakatifu anakaa ndani yetu — *ikiwa* sisi ni Wakristo wa kweli.

Tunda la Roho hutenganisha mfuasi wa Yesu Kristo na ulimwengu usiomcha Mungu, wa uovu, ikifunua nguvu ya ndani ambayo husaidia mfuasi kuwa kama Kristo katika maisha ya kila siku.

Katika mistari iliyotangulia, Paulo aliwasilisha kazi za mwili ambazo zinatofautishwa kabisa kwa tunda la Roho. “Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya; uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo, katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu” (Wagalatia 5:19-21). Hii ni onyo kali sana kutoka kwa Paulo. Anatuambia wazi, sio suala la ikiwa uliokoka au sivyo. Badala yake, alisema, wote wanaoshiriki katika “kazi za mwili” hawautarithi Ufalme.

Mara tu tunapokuwa katika hali ya kuokolewa, dhambi zetu zinafutwa nje ya rekodi, na tunapokea Roho Mtakatifu, tunaweza kuwa na ujasiri kamili kwamba, kama tawi, tumeshikamana kikamilifu na Mzabibu, Yesu Kristo. Hajalishi ni hali gani ya hewa ambayo tunaweza kukutana nayo maishani, maadamu hatutaacha Mzabibu na kunyauka, tunaweza kuwa na hakika tumetiwa muhuri kwa siku ya ukombozi. “Wala msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa ye ye mliitiwa muhuri hata siku ya ukombozi” (Waefeso 4:30).

Uhakikisho wetu wa wokovu upo tu kwa Yesu Kristo. Ni Yesu aliyetuombea, na hiyo ni habari njema. Yesu aliomba sala hii, “Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako, ili wao pia wawe umoja ndani yetu, ili ulimwengu upate kuamini kwamba umenituma. Nami utukufu ulionipa nimewapa wao; ili wawe na umoja, kama sisi tulivyo umoja. mimi ndani yao, na wewe ndani yangu, ili wakamilishwe katika umoja; ili ulimwengu ujue ya kuwa ndiwe ulienituma, ukawapenda wao kama ulivyonipenda mimi” (Yohana 17: 21-23).

Yesu anaomba maombi matatu kwa Baba. Katika ombi la kwanza, Yesu aliomba ombi la umoja — kwamba wangkuwa kitu kimoja. Ombi hili linajumuisha waumini wote wa wakati wote. Umoja huu huonekana zaidi kuititia upendo, utiifu, na kujitolea kwa mapenzi ya Baba.

Katika ombi la pili, Yesu aliombea umoja kati ya waumini ambao unategemea umoja wa Yesu na Baba. Wafuasi wote wa Kristo wanaweza kuunganishwa ikiwa wanaishi kwa umoja na Mungu. Kwa mfano, kila tawi linaloishi kwa umoja na Mzabibu linaunganishwa na matawi yote mengine (ona Yohana 15:1-17); au kila sehemu ya mwili imeunganishwa na sehemu zingine ili wakati mmoja anaumia, wote humquia, na wakati mmoja anafurahi, wote hufurahi (1 Wakorintho 12: 12-27). Muungano huu wa Baba na Mwana ungesababisha watu ulimwenguni kote kuamini kwamba Yesu alikuwa ametumwa na Mungu kama Mwokozi wa ulimwengu — na sio kuamini tu, bali kupokea Mwokozi huyu kama wao. Ombi la tatu la Yesu linatuambia kwamba watu wote wana nafasi ya kushikamana na Mzabibu wa kweli katika maisha yao.

Usichelee kushikamana na Mzabibu wa kweli, Yesu Kristo. Fursa ya wokovu wenye uhakika unakua mfupi kila siku kwa kizazi hiki.

Mti wa Mzeituni Maalum

Tunapata katika Biblia aina nyingi za miti iliyotumiwa kama vielelezo kwa Israeli. “Mzeituni ukiwa kati wa mwiba, mtini, mzabibu, shamba la mizabibu, na mzeituni zitakuwa komamanga.” Kila mti inaelezea sura tofauti ya Israeli. Paulo, katika barua yake kwa Warumi, anatumia picha ya mti wa mzeituni kuonyesha kuwa Israeli hawatakataliwa, lakini watakuwa na wakati ujao mzuri.

Hapo zamani watu wa Kiyahudi walikuwa wamesikia maneno ya kukataliwa. Wakati katika kina cha dhambi yao Mfalme Manase alipotawala ufalme wa kaskazini wa Israeli, Mungu alisema atatupa watu wake kwa sababu ya dhambi zao. “Nami nitawatupa mabaki ya urithi wangu, na kuwatia mikononi mwa adui zao; nao watakuwa nyara na mateka kwa adui zao wote; kwa sababu wametenda yaliyo mabaya machoni pangu, na kunikasirisha, tangu siku ile walipotoka baba zao katika Misri hata leo hivi” (2 Wafalme 21:14-15).

Hata Yeremia alikuwa amewaonya watu kwamba Mungu alikuwa amewatupa. “Zikate nywele zako, Ee Yerusalem, uzipupe, na ukafanye maombolezo juu ya vilele vya milima; kwa maana Bwana amekikataa na kikitupa kizazi cha ghadhabu yake” (Yeremia 7:29).

Kwa swali hili Paulo inaelezea wasiwasi mzito. Je! Mungu alikata tamaa na Israeli na mwishowe akachoka na uasi wao wa kila mara na kuwatupa milele? Jibu la Paulo kwa kweli ni sivyo! Paulo alijadili kwamba alikuwa amepokea wokovu, na alikuwa Myahudi, mzao wa Ibrahim na mtu wa kabile la Benyamini, (Warumi 11:1). Ikiwa Mungu angemtupa mtu ye yeyote hakika ingekuwa Paulo, kwa sababu aliwatesa Wakristo kabla ya kuwa mwamini.

Paulo alijadili, na kwa haki, kwamba Mungu hakuwatupa watu wake katika siku za Musa, au katika siku za manabii. Na hawatupi sasa. “Mungu hakuwasukumia mbali watu wake aliowajua tokeo awali” (Warumi 11:2). Ingawa Israeli iliendelea kutokuwa mwaminifu, Mungu daima hutimiza ahadi zake. Ni Mungu aliyechagua Israeli kuwa watu ambao kuwapitia mataifa mengine yote ya ulimwengu yangemjua. Ilikuwa kwa Ibrahim, Babu wa Israeli ambaye Mungu alifanya ahadi hiyo, na Israeli haikupaswa kufanya chochote ili kuchaguliwa. Akiongea na Ibrahim, Mungu alisema, “Nami nitakufanya wewe kuwa *taifa kubwa*, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka” (Mwanzo 12:2).

Katika kitabu cha Warumi, Paulo anaendelea kuonyesha kujikwaa kwa Israeli, lakini kwa wakati huo huo anaweka wazi kuwa taifa haliko mbali na kuponywa. Upofu wao sio wa kudumu na kuanguka kwao sio mbaya. Kujikwaa kwa Israeli kunamaanisha kwamba wokovu umefikia Mataifa, na Israeli kumkataa Kristo ilikuwa sehemu ya mpango wa Mungu wakati wote

iliyokuwa muhimu kama Chaguo kuu la Mungu la Yakobo juu ya Esau. Wokovu wa Mataifa una kusudi, na kusudi hilo ni *kuwafanya Wayahudi wawe wenyewe vivu*.

Hamu ya Paulo ni kwamba Wayahudi watambue kwamba Mungu aliwabariki sana Mataifa wakati waliamini Masihi wa Wayahudi wenyewe. Wayahudi wanaweza kugundua kwamba baraka hizo hizo zilizotolewa kwa watu wa mataifa zinapatikana kwao kama sehemu ya agano la Mungu, lakini yanaweza kupatikana tu kwa imani katika Yesu Kristo.

Paulo anaamini kwamba kukataa kwa Israeli kumpokea Kristo ni kwa muda tu. Anaelezea hii kwa kutumia kielelezo. Mizizi kwa uwazi, ni sehemu ya kwanza ya mti, na inaunda “mienendo” ya matawi. Imani ya Ibrahim ilikuwa kama mzizi wa mti wenyewe kuzaa, na watu wa Kiyahudi ni matawi ya asili ya mti. Kama matokeo ya chaguo la Mungu na mwitikio wa uaminifu wa Ibrahim, taifa liloshuka kutoka kwake lilikuwa takatifu. Ikiwa mzizi ni mtakatifu, basi tawi lolote linalolishwa na mzizi huo litakuwa takatifu pia.

Ni matawi mengine tu yaliyovunjwa kutoka kwa mti, kwa sababu ya dhambi na kutokuamini. Matawi haya yaliyovunjika ni Wayahudi wasioamini. Katika nafasi yao, Mataifa ambayo Paulo analinganisha na matawi ya mzeituni mwitu, yamepandikizwa. Paulo awaonya watu wa mataifa, “shina la mizeituni mwitu” ambao umepandikizwa kwenye mzeituni uliopandwa (Israeli), sio kwa kiburi au kujisifu, kwani inawezekana kuziondoa, na inawezekana kwa matawi yao ya asili kupandikizwa tena. Akiongea juu ya Israeli, Paulo alisema, “Nao hao pia, wasipokaa katika kutokuamini kwao, watapandikizwa; kwa kuwa Mungu aweza kuwapandikiza tena” (Warumi 11:23).

Tunakuwa sehemu ya “mti” wa Mungu kwa imani. Ikiwa sio kwa imani, tunapoteza uwezo wowote wa uhusiano na Mungu kwa kutokuamini. Mataifa hupandikizwa kwa neema katika familia ya Mungu. Myahudi mpotovu anayegundua imani ya Ibrahim anakuja nyumbani. “Kwa maana ikiwa wewe ulikatwa ukatolewa katika mzeituni, ulio mzeituni mwitu kwa asili yake, kisha ukapandikizwa, kinyume cha asili katika mzeituni ulio mwema; si zaidi sana wale walio wa asili kuweza kupandikizwa katika mzeituni wao wenyewe?” (Warumi 11:24).

Mungu hatumii mzeituni bila sababu. Mzeituni kama picha ya Israeli inaonyesha siku za usoni nzuri zaidi. Mzeituni ni moja ya miti yenyewe thamani zaidi katika Palestina ya zamani. Mara nyingi ulikuwa mti pekee wa saizi yoyote katika eneo hilo. Iliitwa “mfalme” wa miti (Waamuzi 9:8), dalili ya umuhimu wake wa kiuchumi wa zamani.

Mzeituni unaashiria uzuri, nguvu, na amani. Zaburi inarejelea kuzaa matunda kwake. “Mkeo atakuwa kama mzabibu uzao, vyumbani mwa nyumba yako. Wanao kama miche ya mizeituni, wakiizunguka meza yako” (Zaburi 128:3). Hosea anazungumzia uzuri wa Israeli, “Matawi yake yatatandaa, na uzuri wake utakuwa kama uzuri wa mzeituni, na harufu yake kama Lebanoni” (Hosea 14:6).

Mzeituni ni maalum sana kwa njia nyingi. Ina matawi mengi na mizizi na imejikunyata. Inakua hadi iwe kizee sana na inaweza kuzidi kukua tena kupertia kupogoa. Haina pete za mwaka, na hubakia kijani kibichi kila mwaka.

Mungu alichagua taifa la Israeli, na hajawahi kulitupa. “Hivyo Israeli wote wataokoka; kama ilivyoandikwa, Mwokozi atakuja kutoka Sayuni; Atamtenga Yakobo na maasia yake. Na hilo ndilo agano langu nao, nitakapowaondolea dhambi zao” (Warumi 11:26-27).

Wengi wanaamini kwamba kifungu “Israeli wote wataokoka” inamaanisha kuwa Wayahudi wengi katika kizazi cha mwisho kabla ya kurudi kwa Kristo watamgeukia Kristo kwa wokovu. Wengine wanaamini Paulo anatumia neno *Israeli* kurejelea taifa “la kiroho” la Israeli, ambalo linajumuisha Wayahudi na watu wa mataifa waliopokea wokovu kwa njia ya imani katika Kristo. Kwa hivyo, “Israeli yote,” au waamini wote, watapokea zawadi ya Mungu ya wokovu iliyohidiwa. Na bado wengine wanaamini kwamba kifungu hicho kinamaanisha kuwa Israeli kwa jumla watakuwa na jukumu katika Ufalme wa Kristo, kwamba utambulisho wa Wayahudi kama watu hautatupiliwa mbali, kwani Mungu alichagua taifa la Israeli, na hajawahi kamwe kuitupa. Huu ndio kuelewa bora, kwani Mungu pia alichagua kanisa, kupertia Yesu Kristo, naye hataitupa kamwe. Hii haimaanishi kuwa kikundi chochote kina wokovu usiofaa. Kila mtu lazima awe mwaminifu na kukua daima katika neema na maarifa ya Yesu Kristo, asili yao ya dhambi ikishindwa na Roho Mtakatifu anayekaa ndani yao.

Kusudi la Paulo ni kuonyesha kwamba Mungu hakuwa ameitupa Israeli. Kweli, Paulo aliamini taifa la Israeli litarejeshwa kwa Mungu. Wayahudi na watu wa mataifa watafanywa kuwa mti unaostawi unaowakilisha Ufalme, na vile vile rundo lililovunjika matawi yaliyoandaliwa kwa kuchomwa moto ambayo inawakilisha wale ambao kwa bahati mbaya wamekataa neema na msamaha uliotolewa na Mungu.

Paulo ananukuu kutoka kwa Isaya 59:20-21: “Na Mkombozi atakuja Sayuni, kwao waachao maasi yao katika Yakobo, asema BWANA.” Yesu Kristo ndiye mkombozi atakayekuja kutoka Yerusalem. Pia dhambi zao zitaondolewa (Yeremia 31:33-34). Hakika, kila mtu wakati huo atamjua Bwana, na dhambi zao zitasahauliwa.

Mungu yuko tayari kabisa kuwahurumia wote wanaomjia. Isaya 60 inafunua picha nzuri ya Wayahudi na watu wa mataifa wakipata baraka nyingi za Mungu.

Mzeituni pia umeunganishwa kwa *kurudi* kwa Yesu Kristo, kwa kuwa wakati Bwana atarudi Israeli itarudi kwenye Mlima wa Mizeituni. “Na siku hiyo miguu yake itasimama juu ya mlima wa Mizeituni, unaoelekea Yerusalem upande wa mashariki, nao mlima wa Mizeituni utapasuka katikati yake, upande wa mashariki na upande wa magharibi, litakuwako huko bonde kubwa sana; na nusu ya mlima ule utaondoka kwenda upande wa kaskazini, na nusu yake utaondoka kwenda upande wa kusini” (Zekaria 14:4).

Utukufu wa Mungu uliondoka Hekaluni na haukuwapo tena kabisa hadi Kristo mwenyewe aliitembelea katika nyakati za Agano Jipy. Ezekieli, katika maono, alitazama utukufu wa Bwana ukiondoka mjini: “Utukufu wa BWANA ukapaa juu toka katikati ya mji, ukasimama juu ya mlima wa upande wa mashariki” (Ezekiel 11:23). Tena katika roho, Ezekieli anaona kurudi kwa utukufu wa Mungu: “Na tazama, huo utukufu wa Mungu wa Israeli ultokea kwa njia ya mashariki; na sauti yake ilikuwa kama mshindo wa maji mengi, nayo nchi iling’aa kwa utukufu wake. Na maono niliyoyaona yalikuwa kama maono niliyoyaona nilipokuja kuuharibu mji; nayo maono niliyoyaona yalikuwa kama maono niliyoyaona na mto wa Kebari; nikaanguka kifudifudi. Na huo utukufu wa BWANA ukaingia ndani ya nyumba kwa njia ya lango lile lielekealo upande wa mashariki” (Ezekiel 43:2-4).

Lazima ilikuwa mbaya sana kwa Ezekieli wakati utukufu wa Mungu ulipoondoka Hekaluni; na sasa alipoona ikirudi aliingiwa na hofu na furaha kupita uwezo wake wa kuelezea. Mistari hii inamaanisha kwamba Mungu atarudi vile alivyoondoka.

Ishara ya uharibifu wa mji na Hekalu ilitolewa na kuondoka kwa Mungu. Sasa, ili Mungu arudi, masharti Yake lazima yatimizwe: Ibada ya sanamu ilibidi iondolewe. Ezekieli anaweza kuwa akiwaamuru watu kujenga Hekalu kulingana na maagizo aliyyapokea kutoka kwa malaika mbunifu, lakini watu hawakutubu kamwe na masharti za Mungu hazikutimizwa, kwa hivyo utimizo haukutokea.

Katika kitabu cha Matendo itapatikana taarifa ya mwisho ya Kristo hapa duniani: “Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalem, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi” (Matendo 1:8). Baada ya kutoa maagizo haya muhimu, wanafunzi walimwona Yesu akipaa juu angani na kupotea ndani ya wingu. Wingu hili lilikuwa mfano wa utukufu wa Mungu. Wingu pia lilimfunika Yesu na wanafunzi wake watatu wakati wa kubadilika (Luka 9:34-35).

Ilikuwa muhimu kwa wanafunzi kumwona Yesu akifanya mabadiliko haya. Kupaa kuliwathibitishia kwamba Yesu kwa kweli alikuwa Mungu. Walipokuwa wakimwangalia akipotea, viumbe wawili wa malaika walitokea. Waliwaambia wanafunzi kwamba siku moja, kama vile mlivyoona akienda, atarudi. Kwa hakika, itakuwa kwenye Mlima wa Mizeituni.

Mlima wa Mizeituni ni “mlima wa upande wa mashariki wa mji” wa Yerusalem (Ezekiel 11:23). Bonde la Kedroni lenye urefu wa nusu maili pekee hutenganisha Jiji Takatifu kutoka Mlima Mtakatifu. Kwa kweli kuna mikutano mitatu yenyе alama tofauti, yenyе mviringo: Mlima Scopus kwa upande wa kaskazini, Mlima wa Makosa upande wa kusini, na Mlima wa Mizeituni ukiwa katikati. Inasimama futi 2,680 juu ya usawa wa bahari, ambayo inamaanisha kwamba iko na urefu wa futi 200 kuliko eneo la Hekalu huko Yerusalem.

Kwenye sehemu kuu ya mkutano huo kuna mabaki ya kile kinachoitwa “Kanisa la Kupaa,” ya kiasili lililojengwa wakati wa karne ya nne na fedha zilizotolewa na Maliki Konstantino. Katika miaka ya hivi karibuni, makaburi ya zamani yamegunduliwa karibu na mahali pa jadi ambapo

Yesu alilia juu ya Yerusalem. P.B Bagatti amechunguza makaburi, na kulingana na hesabu yake mahali pa mazishi palitumika wakati wa karne ya kwanza BK, na pia katika karne ya tatu na ya nne. Vyombo (masanduku ya mazishi) vingine thelathini na sita vilipatikana na vilikuwa vya karne ya kwanza. Yaliyoandikwa juu ya haya ni majina kama Jarius, Simon Bar-Yona, Mary, Martha, na Siloam. Chombo kimoja linalo jina la “Yuda aliyegeuza imani wa Tiro.”

Kuzaa Matunda Mema

“Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki, wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi barazani pa wenye mzaha. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki; na kila alitendayo litafanikiwa” (Zaburi 1:1-3).

Kuna hekima rahisi sana katika aya hizi. Tunapotumia hekima ya Mungu, matunda (matokeo au mazao) tunayozaa yatakuwa mazuri na tutapata kibali cha Mungu. Kama vile mti huloweka maji na kuzaa matunda mazuri, sisi pia tunapaswa kuloweka kwa Neno la Mungu, tukizalisha matendo na mitazamo inayomheshimu Mungu. Ili kufanikisha chochote cha maana, lazima tuwe na neno la Mungu miyoni mwetu.

Maandishi: Loren M. Chamberlain

Tafsiri: Elijah Ogeda